**MKATABA WA UPANGISHAJI**

**MKATABA** huu umeingiwa leo hii tarehe 01 mwezi 12, 20 23.

**KATI YA**

**BI KELTA MALUGU** wa S. L. P. 4216 Dar es Salaam (ambaye katika mkataba huu anajulika kama **"MPANGISHAJI"**) kwa upande mmoja.

**NA**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEAT)** wa S. L. P 11430 Dar es Salaam (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama **"MPANGAJI"**) kwa upande mmoja.

CERTIFIED TRUE COPY OF THE ORIGINAL
JANE GERALD
ADVOCATE, NOTARY PUBLIC &
COMMISSIONER FOR OATHS
Sign:...... Date: 24/04/2024

**UMEANDALIWA NA:-**

**Pande zote Mbili**

**MKATABA WA UPANGISHAJI**

**MKATABA** huu umefanyika leo tarehe ___01___ mwezi ___12___, 20 23.

**KATI YA**

**BI KELTA MALUGU** wa S. L. P. 4216 Dar es Salaaam, (ambaye kwa minajili ya mkataba huu anajulikana kama **"MPANGISHAJI"** tamko ambalo mazingira yake yakiruhusu litahusisha washiriki/wafuasi wake wateuliwa ama warithi wake halali) kwa upande Mmoja wa mkataba huu.

**NA**

**THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEAT)** wa S. L. P. 11430 Dar es Salaam, kampuni iliyosajiliwa kwa sheria za Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (ambayo kwa minajili ya Mkataba huu itajulikana kama **"MPANGAJI"** tamko ambalo mazingira yake yakiruhusu litahusisha washiriki/wafuasi wake wateuliwa ama warithi wake halali) kwa upande wa pili wa mkataba huu.

**KWAMBA,** Mpangishaji ni Mmiliki halali wa eneo ambalo halijapimwa lenye **nyumba namba** KPU/A/407 eneo la mtaa wa **Kipunguni A, Kata ya Kipawa, Wilaya ya Ilala, Jiji la Dar es Salaam.**

**NA KWAMBA,** Mpangishaji kwa hiari yake na bila ya kushawishiwa au kulazimishwa na mtu yoyote ameamua kumpangisha mpangaji eneo lake kwa ajili ya shughuli mabalimbali za kiuchumi ikiwa ni pamoja na uuzaji wa bidhaa anazozalisha na shughuli za kiofisi na Mpangishaji amekubali kupangishwa nyumba hiyo kwa bei ambayo wamekubaliana.

**HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:**

1. Kwamba kodi ya eneo hilo ni **TZS 150,000.00 (Shilingi za Kitanzania Laki Moja na Elfu Hamsini Tu)** kwa kila mwezi.
2. Kwamba mpangishaji amekubali kumpangishia mpangaji eneo tajwa hapo juu kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya kalenda kuanzia tarehe 01-12-2023 na kumalizika tarehe 30/11/2028.
3. Kwamba Mpangaji atamlipa Mpangishaji pesa ya pango ya miezi mitatu (3) yaani **TZS 450,000.00 (Shilingi za Kitanzania Laki Nne na Elfu Hamsini Tu)** siku ya kusaini mkataba huu na mfumo wa malipo utakuwa kila baada ya miezi mitatu.
4. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa mpangaji atalipia malipo ya umeme, maji safi (water bills), maji taka, ulinzi na gharama nyingine zitakazojitokeza kwa ujumla kulingana na matumizi yake.
5. Kwamba mkataba huu unashuhudia kuwa mpangaji atagharamia utoaji wa taka zake mwenyewe.
6. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa mpangaji ataweka eneo katika hali ya usafi kwa muda wote wa upangaji wake.

CERTIFIED TRUE COPY OF THE ORIGINAL
JANE GERALD
ADVOCATE, NOTARY PUBLIC &
COMMISSIONER FOR OATHS
Sign:.......... Date: 24/04/2024

7. Kwamba mpangaji anaruhusiwa kumpangishia mtu mwingine na anaweza kufanya marekebisho mbalimbali kwenye eneo tajwa hapo juu na atamtaarifu mpangishaji kabla ya kuanza marekebisho hayo au upangaji huo.

8. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa mpangaji haruhusiwi kuleta wala kuingiza vitu hatari vinavyoweza kulipua au kusababisha mlipuko katika eneo hilo la upangaji.

9. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa Mpangishaji ana haki ya kukagua eneo lake ili mradi atoe taarifa kwa mpangaji au wahusika wake.

10. Kwamba mkataba huu unashuhudia kuwa mpangaji ana haki ya kufurahia upangaji wake katika nyumba tajwa kwa kipindi chote cha upangaji wake.

11. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa mpangaji anaweza kuongeza muda wa upangaji wake kwa masharti haya au mapya kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa mpangishaji Miezi mitatu (3) kabla ya makataba kumalizika, vivyo hivyo mpangishaji anaweza kutoa notisi ya kuhama miezi mitatu kabla ya mkataba kuisha.

12. Kwamba mkataba huu unashuudia kuwa upande wowote unaweza kuvunja mkataba huu ili mradi uwe tayari kulipa fidia na gharama za kuvunja mkataba.

13. Kwamba kama mpangishaji hatapenda kuendelea na mkataba na mpangaji, basi atatoa NOTISI ya Miezi mitatu (3) kabla ya mkataba kwisha. Na kama mpangaji ataamua kuondoka yeye mwenyewe kwa hiari yake, mpa-ngishaji hatarudisha fungu la pango litakalobaki.

14. Endapo kutatokea mgogoro kati ya mpangaji na mpangishaji, mgogoro huo **utasuluhishwa baina yao** kama suluhu haitapatikana, mgogoro huo utawasilishwa kwenye **baraza la ardhi** na kufuata utaratibu wa kawaida wa sheria baada ya hapo.

15. Mkataba huu unaongozwa na sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA USHUHUDA wa makubaliano hayo pande zote mbili zimetia sahihi kama ilivyo hapa chini;

**UMESAINIWA** na kutolewa Dar es Salaam na
**BI KELTA MALUGU** ambaye
namfahamu/~~ametambulishwa kwangu~~ na
______________________________
leo tarehe 01 mwezi 12, 2023

} Malugu
**MPANGISHAJI**

MBELE YANGU:
JINA: JANE GERALD
SAHIHI: [signature]
ANUANI: S.L.P. 11430 DSM
CHEO: MTHIBITISHAJI WA UMMA

Jane Gerald
Box 11430 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

CERTIFIED TRUE COPY OF THE ORIGINAL
JANE GERALD
ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS
Sign: ........ Date: 29/01/2024

**UMESAINIWA** na kutolewa Dar es Salaam na
FURGENCE MATHIAS FURAHA

Kwa niaba ya **THE REGISTERED TRUSTEES OF TANZANIA COMMUNITY EMPOWERMENT ASSOCIATION (TANCEAT)**
ambaye namfahamu/ametambulishwa kwangu na
______________________

leo tarehe 01 mwezi 12, 2023

_______________
**MPANGAJI**

**MBELE YANGU:**
**JINA:** JANE GERALD
**SAHIHI:** ______________
**ANUANI:** S.L.P. 11430 DSM

Jane Gerald
Box 11430 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

CERTIFIED TRUE COPY OF THE ORIGINAL
JANE GERALD
ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS
Sign:............ Date: 24/04/2024